WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# KANUNI MPYA ZA TOZO ZA UVUVI 2020



*"Natoa wito kwa Wataalam wa Sekta ya Uvuvi kuhakikisha wanasimamia vyema na kwa weledi Utekelezaji wa Kanuni hizi za Tozo "-* **Dkt. Rashid Tamatamah, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)**



## MAREKEBISHO YA TOZO GN 491A ya Mwaka 2020

| TOZO | MAREKEBISHO YAKE |
|---|---|
| Gharama za leseni za kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi. | Zimeshuka kutoka Dola 2500 hadi Dola 500 kwa mazao ya uvuvi katika maji chumvi (Pweza, Ngisi, Kambakochi, Kaa, Kambamiti) kwa wafanyabiashara wadogo. |
| Ada ya leseni za kusafirisha dagaa. | Imepungua kutoka Dola 1000 hadi Dola 250<br>• Kwa dagaa wa maji chumvi na maji baridi.<br><br>Leseni nyingine zilizopungua ni pamoja na:<br>• leseni za kujishughulisha na uchakataji wa mabondo,<br>• biashara ya Simbi, na Mwani,<br>• usafirishaji wa samaki wakavu, samaki wabichi, samaki wa mapambo na samaki aina ya sangara aliyetolewa matumbo. |
| Tozo za kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi (export royalty) | Zimepungua;<br>• Kutoka dola 0.2 hadi dola 0.16 kwa kila kilo kwa dagaa wa kutoka Ziwa Victoria,<br>• kutoka dola 0.3 kwa dagaa wa Ziwa Nyasa na maji chumvi hadi kufikia dola 0.16, na<br>• kutoka dola 1.0 hadi dola 0.5 kwa kilo kwa dagaa wa Ziwa Tanganyika. |
| Ushuru wa kusafirisha minofu ya Sangara kwenda nje ya nchi. | Umepungua kutoka dola 0.24 hadi dola 0.2 kwa kila kilo. |

Imetolewa na

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**www.mifugouvuvi.go.tz**
**Simu: 0763 255255**